TANGAZO LA SERIKALI NA. 204 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 413 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3-

(a) katika tafsiri ya neno "afisa mwidhiniwa", kwa kuingiza maneno "na Mkurugenzi" katikati ya maneno "atakayeteuliwa" na "kusimamia";
(b) kwa kufuta tafsiri ya msamiati "choo bora"; na
(c) kwa kuongeza kulingana na mpangilio wa kialphabeti tafsiri ya msamiati mpya kama ifuatavyo:

Sura ya 191

""choo" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;".

Marekebisho ya kanuni ya 15

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 15(3) kwa kufuta maneno "tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi" na badala yake kuweka maneno "tarehe ya mwisho wa mwezi".

Marekebisho ya kanuni ya 48

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 48 kwa-

(a) kufuta aya (l); na

(b) kubadili mpangilio wa aya (m) hadi (w) kuwa aya (l) hadi (v) mtawalia.

Dodoma,
10 Januari, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri Wa Nchi – OR-TAMISEMI*